

# *IMANI*

 Lakini inakubidi kutumia imani katika Mungu, kuifanya itende kazi. Unaona? Kwa hiyo una ufuluo wako mwenyewe ndani yako. Ufuluo wako unakaa ndani yako, katika roho yako.

<sup>2</sup> Sasa, unajua, Yesu alipokufa msalabani, “Nafsi Yake ilishuka kuzimuni ikawahubiri nafsi waliokuwa kifungoni, wale ambao hawakutubu katika siku za uvumilivu wa Nuhu.” Mwili Wake uliingia kaburini. Lakini, kabla Yeye hajafa, aliiakabidhi Roho Yake mkononi mwa Mungu. Mkononi . . . “Katika mikono Yako naiweka Roho Yangu.” Kwa hiyo, unaona, Roho Yake ilienda kwa Mungu; nafsi Yake ikaenda kuzimuni; mwili Wake ukaenda kaburini.

<sup>3</sup> Sasa, hiyo Roho iliyokuwa ndani Yake ilikuwa ni Roho ya Mungu. “Roho hiyo, zamani za kale na kwa njia mbalimbali, iliwatia upako manabii, wapate kuwalettea watu Ujumbe; katika siku za mwisho, kupitia Kristo; na sasa, katika siku hizi hapa, kupitia Injili.” Sasa, tunapompokea Kristo moyoni mwetu, hayo hapo yote tunayohitaji. Huo hapo Uzima wa Milele.

<sup>4</sup> Sasa, Kristo asingeweza kurudi mpaka siku tatu zilipotimia. Kwa sababu, Roho Yake ilikuwa nyuma ya kiwambo, kama kizuizi, namna *hii*, hata asingeweza kukivuka kizuizi hicho, kwa sababu kilikuwa ni Neno la Mungu lilionenwa, kwamba, “Alikuwa akae kaburini kwa muda wa siku tatu mchana na siku tatu usiku.” Sasa, Yeye asingeweza kurudi mpaka hizo siku tatu mchana na usiku zilipokwisha. Ndipo hapo siku tatu mchana na usiku zilipokwisha, Roho Yake iliachiliwa. Ikaenda moja kwa moja kwenye nafsi Yake, Nayu nafsi yake ikarudi na kuuchukua mwili, na kutimiza kile alichosema. “Ninao uweza wa kuutoa Uhai Wangu. Ninao uweza wa kuutwaa tena. Ninao uweza.”

<sup>5</sup> Sasa, kila mmoja wenu anao uweza, kwa njia ile ile, kwa kuwa ninyi ni wana na binti za Mungu. Na Roho yeye yule aliye ndani yenu, asubuhi ya leo, Roho Mtakatifu aliye ndani yenu asubuhi ya leo, Roho Mtakatifu yuyo huyo atakufufua. Kwa hiyo, wewe una uweza wa kujifufua tena.

<sup>6</sup> Ukifa, nafsi yako itaenda kwenye ninii—ninii . . . chini ya madhabahu ya Mungu, sio katika . . . moja kwa moja Mbele za Mungu. Sasa, roho yako itaenda kwa Mungu, bali huwezi kurudi. Kumbukeni, katika Biblia, ilisema roho . . . “Nafsi chini ya madhabahu, wakilia, ‘Bwana, hata lini, hata lini?’” Wala wasingeweza kurudi mpaka Maandiko yatimie, na, kama Kristo, wasingeweza kurudi mpaka Maandiko yatimie. Ndipo, baada ya ninii, yote yaliyokuwa yamefanywa, mateso yote yamekwisha, nao ndugu hao wameteseka kwa mambo yale yale, ama tumeteseka kama wao walivyoteseka, na kadhalika; basi,

kwenye siku hiyo, utajua mahali hasa ulipozikwa, roho yako itaachiliwa kutoka kwa Mungu nayo itakuja kwenye nafsi hiyo.

<sup>7</sup> Sasa, nafsi ni ile sehemu yako inayojua na kufahamu, akili yako. Mnakumbuka ono nililokuwa nalo sio muda mrefu uliopita, ama kuhamishwa kule kudogo, nikaenda mahali pale na kuwaona hao watu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, roho yako itarudi kwenye huo mwili, na mwili wa namna hi—hiyo, nafsi, ambayo ni mwili ambao hauna haja ya kula na kadhalika. "Maskani hii iliyo ya dunia ikiharibiwa, tuna moja inayongoja tayari," mwili wa kimbunguni. Na kwa huyo roho, na hiyo nafsi na mwili wa kimbunguni, utaufufua tena mwili huu wa kawaida kwa ajili ya ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Unaona? Unao uweza ndani yako sasa, kufanya jambo hilo, sasa. Lakini, uweza huo ulio nao ndani yako sasa, ungeweza kuufanya ulimwengu mpya. Mungu hana sehemu ndogo, dhaifu; na sehemu kubwa, nzito ambazo zina nguvu. Mguso ulio mdogo sana wa Mungu una nguvu zote, unaona, mguso ulio mdogo sana wa Mungu. Kwa hiyo, mwajua.

Kwa hiyo ninajaribu kuwaweka katika imani sasa.

<sup>8</sup> Unajua kwamba jambo fulani limekupata, kama Mkristo. Unajua? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ulikuwa ukielea *hapa* chini katika vinyaa, ukiwa na vinyaa vyote na dhambi, na kunywa pombe, na kucheza kamari, na—na mambo ya ulimwengu. Vema, mara ulipoamini ya kwamba Kristo amekusamehe dhambi zako, uliinuka juu ya upuuzi huo. Sasa unaelea *hapa* juu, unaona, juu ya yote hayo. Kwa nini? Kwa sababu wewe unaamini ya kwamba u Mkristo. Ndipo wakati ulipomkubali Kristo, na Roho Mtakatifu akaja kwako, basi una imani na Roho Mtakatifu, hiyo inakupa uweza wa kuelea juu ya maisha ya aina hiyo ya dhambi.

<sup>9</sup> Vema, sasa, jambo pekee linalokupasa kufanya, kuelea juu zaidi katika uponyaji, kuwa tu na imani zaidi, ninii tu—endelea tu kuisukuma. Unaona? Na haya basi. Sasa basi wewe ni mgonjwa, nawe si Mkristo, kuwa Mkristo sasa hivi, ili kwamba hizo nguvu za uponyaji zitakuja ndani yako, kwa kuwa Mkristo. Na hiyo itakupa imani kuelea juu ya dhambi. Itakupa imani. Na kila kitu unachohitaji, katika safari hii, kimo mumo humo ndani yako sasa. Na jambo pekee unalopaswa kufanya ni kumwamini Mungu, hilo linasukuma hayo mambo mazuri kutoka ndani yako, ambayo yamo ndani yako, kwa Roho Mtakatifu. Mnaelewa dhahiri sasa? Mmelipata? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

<sup>10</sup> Ninaamini Billy aliniambia, jana usiku, alinipigia simu na kusema, "Njoo, asubuhi ya leo, hasa sana kwa ajili ya mtu mmoja aliyekuja, akifikiri tunafanya ibada juma hili, za hiyo Mihuri Saba." Nao wakamleta mtoto mgonjwa, ninaamini. Na endapo upo hapa sasa, bwana, kumbuka, huwezi... Ninii yako—imani

yako itabidi imwendee mtoto huyo, kama ni—kama ni maskini mtoto mdogo, mchanga.

<sup>11</sup> Lakini sasa hebu nichukue Andiko lingine, kama ni sawa, kwa muda mfupi tu. [Ndugu Neville anajibu, “Endelea moja kwa moja, ndugu. Amina.”—Mh.]

<sup>12</sup> Kumbukeni tu, sasa, katika Injili, tunasoma katika mlango wa 16, ninaamini, wa Matendo, ambapo kwamba Paulo na Sila walikuwa gerezani usiku mmoja. Nao walikuwa wamepigwa kwa kuwa walikuwa wamemtoa pepo kutoka kwenye msichana mwaguzi. Nay o ilikuwa ni...Na, yeye, bwana zake walikuwa wamekasirishwa na jambo hilo. Nao wakawapiga, wakawaingiza kwenye magereza ya ndani. Na walipofanya hivyo, wakati Paulo na Sila walipokuwa wakiomba, ndipo Mungu alituma tetemeko la ardhi na kuitikisa gereza sana.

<sup>13</sup> Yule mlinzi wa jela Mfilipi, akiwa ni akida, ambapo, kuwapoteza wafungwa wa—wake, ingechukua maisha yake mwenyewe kulipia wafungwa hao. Aliuchomoa upanga wake na alikuwa akitaka kujiua, wakati Paulo alipokimbia hapo na kusema, “Usijidhuru. Sisi sote tupo hapa.”

<sup>14</sup> Naye huyu akida alikuwa na, tuseme, dhana waliyokuwa nayo kumhusu Paulo na hao wengine. Huenda waliimba nyimbo. Huenda walishuhudia, ama kufanya jambo fulani. Lakini, chochote kile, walijua ya kwamba walikuwa ni watu watakatifu. Walijua ya kwamba kulikuwako na jambo tofauti kuwahusu hao watu. Kwa sababu, upesi, yeye aliluliza, “Nifanye nini nipate kuokolewa? Nifanye nini nipate kuokolewa?”

<sup>15</sup> Sasa, Paulo alisema, “Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe pamoja na nyumba yako mtaokolewa.”

<sup>16</sup> Vema, sasa, kama kumwamini Bwana Yesu Kristo...Hiyo haimaanishi ya kwamba wokovu *wake ungeiokoa* nyumba yake. Lakini kama anayo imani ya kutosha kumwamini Mungu kwa ajili ya wokovu wake, anaweza kuwa na imani iyo hiyo kwa ajili ya nyumba yake. Nay o nyumba yake haina budi kuingia, mnaona, jambo lile lile.

<sup>17</sup> Kama vile Ayubu alivyofanya, kama nilivyo sema hivi majuzi usiku, huko Georgia, mkutanoni. Nilisema, “Ayubu, yeye alisema, ‘Sasa, sijui kama watoto wangu wametenda dhambi, lakini vi pi kama wametenda dhambi?’” Naye Ayubu alikuwa na jambo moja la kufanya, apate kuwa mwenye haki, hilo lilikuwa, kutoa sadaka ya kuteketezwa. Alisema angetoa sadaka ya kuteketezwa, kama watoto wake walikuwa wametenda dhambi, basi wangesamehewa dhambi yao. Na ni jambo zuri ambalo huyo baba alifanya. Huyo ni baba mwenye mawazo mema. Tunahitaji baba wengi zaidi wa aina hiyo leo. Ndipo Ayubu akatoa sadaka ya kuteketezwa. Hiyo ni kabla msiba wake haujaanza.

<sup>18</sup> Lakini wakati watoto wake wote walipouawa, na kondoo wake wote wakaangamizwa, na yote aliyokuwa nayo, yakachukuliwa, alikuwa ameketi kwenye lundo la majivu nyuma ya nyumba yake, akijikwaruza kwa kipande cha kigae.

<sup>19</sup> Hivi mliona, baada ya siku za msiba wake, wakati Mungu alipoanza kumrejeshea tena? Ambapo alikuwa na ng'ombe elfu kumi, na kadhalika, Yeye alirejesha maradufu. Na kondoo wake maradufu, na kila kitu maradufu. Lakini mliona? Na Mungu pia akampa Ayubu watoto wake saba. Uliwahi kuwazia mahali walipokuwa? Hiyo sadaka ya kuteketezwa iliwatetea. Waliokolewa, Utukufuni, wakimngojea aje. Yeye yuko pamoja nao leo hii. "Wewe na nyumba yako mtaokolewa." Unaona? Sasa, Ayubu alikuwa na jambo moja la kufanya, kuwa mwenye haki, lilikuwa ni kutoa sadaka ya kuteketezwa.

<sup>20</sup> Una jambo moja la kufanya, kuwa mwenye haki, hilo ni, kumwamini Mungu. Kwa kuwa, kwa imani unaokolewa, kwa imani unaponywa, kwa imani unapata kila kitu ulicho nacho. Unaona? Ni kwa imani, kwamba unaliamini. Sasa, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe pamoja na nyumba yako mtaokolewa."

<sup>21</sup> Sasa, bwana, kama una mtoto huyo mchanga hapa kuombewa, wewe amini, mwenyewe. Nipo hapa kuiweka imani yangu pamoja na yako, nasi tutaamini, pamoja, ya kwamba Mungu atamponya mtoto huyo.

<sup>22</sup> Unaona, tunao ndani yetu uweza wa kufanya jambo hilo. Una ndani yako uweza wa kulifanya. Kila Mkristo ana uweza wa kulifanya hilo. Lakini sasa kama tunaweza tu kupata... Uweza huo unaongozwa na kanuni fulani.

<sup>23</sup> Kama vile nimesema mara nyingi, ni kama vile mvutano unavyoyadhibiti maji, kwa maana ni kanuni. Mvutano huyadhibiti maji.

<sup>24</sup> Jua, linaongozwa na ninii—na ninii... ama dunia, mzunguko wa dunia. Kamwe huwezi tu kulifanya jua lifanye jambo moja, kisha useme, "Ninaamini ninataka kulala kidogo zaidi. Tulia kwa saa moja." Halitafanya hivyo, unaona, kwa kuwa kuna kanuni fulani. Kama utatenda kazi kulingana na kanuni hiyo, vema, basi, kila kitu kitakuwa shwari. Kama utaenda kulala kwa wakati unaofaa, unawenza kuamka katika wakati mzuri. Na kama ukininii... .

<sup>25</sup> Kama vile tulivyo na Ziwa Superior, Ziwa Ontario, Ziwa Huron, na hayo Maziwa Makubwa yote hapa juu. Tuna makumi elfu mara maelfu ya ekari za mashamba huko Nevada, na California, na Arizona, na New Mexico, ambayo yanaungua kabisa, kwa ukosefu wa maji, ya mashamba ambayo yangekuza chochote kile. Ungaliweza kuulisha ulimwengu mzima, huko nje, kama tu ungaliyachukua haya maji, hapa juu, uyapeleke kule chini. Wala halingeyaathiri hayo, kwa sababu yanatokana na chemchemi. Mara tu yakinolewa, yanarudia tu usawa wake

tena, kwa maana mvutano unayashikilia pale. Vema, sasa, kama unaweza kutenda kazi kulingana na kanuni ya mvutano, unaweza kuyachukua haya Maziwa Makuu yote na kunyunyizia hiyo nchi nzima huko, na kuulisha ulimwengu mzima, hakuna mtu angalikosa chakula. Bali huwezi kuketi hapa na kusema, "Naam. Ninaliona. Hakika." Inakubidi kwenda na kulifanya.

<sup>26</sup> Vema, hivyo ndivyo ilivyo na kanuni ya Mungu. Kanuni ya Mungu ni imani. Nasi tuna imani hapa, asubuhi ya leo, kuponya maradhi yoyote, kufanya lolote. Lakini inaongozwa na kanuni fulani, na kanuni hiyo ni imani. Kanuni ya Mungu ni imani. Yesu alisema, "Lolote mtakalo, mnapoomba, kama mnaweza kuamini mmelipokea, litakuwa lenu." Haya basi. Kwa hiyo, imani ndiyo inayoliongoza, nasi tunapewa imani kulingana na vile tunavyoihitaji. Sasa, inatubidi kuninii... Mungu hugawia baadhi yetu imani fulani, wengine imani nyingine. Sio uweza fulani mkuu wa kimbunguni ulio nao. Kwa sababu, unapokuwa Mkristo, wewe—wewe tayari una uweza, bali huna imani ya kuutia huo uweza kazini.

<sup>27</sup> Kwa hiyo sasa, asubuhi ya leo, mnapokuja kuombewa, kumbukeni, Biblia imesema jambo hili. Hii ni kweli. Yakobo 5:14, "Akiwapo mtu wa kwenu, mgonjwa, na awaite wazee wa kanisa. Na wampake mafuta, na kuwaombea. Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, Naye Mungu atamwinua." Ni ahadi, kama utaiamini. Kwa hiyo, unaona, uponyaji umegawiwa mtu binafsi.

<sup>28</sup> Ilikuwa katika siku za Yesu wa Nazareti. Yeye asingeweza kuwaponya watu kinyume na ninii yao—kinyume na imani yao wenyewe. Yeye alisema, "Ninaweza, kama unaamini. Kama unaamini kwamba ninaweza kufanya hili, ninaweza kulifanya." Kama unaweza kuliamini!

<sup>29</sup> Kwa hiyo, baadhi ya watu hutupa ninii—huwatupia wengine uweza wa uponyaji, wainjilisti. Si hivyo. Uweza wa uponyaji umo ndani yako. Umo ndani yako. Wao wanaweka tu gari mbele ya farasi. Mwinjilisti huyo hana uweza wa kuponya.

<sup>30</sup> Roho Mtakatifu Ndiye aliye na uweza wa kuponya, nawe una Roho Mtakatifu. Huo ndio mti ule mdogo ulio wewe, na mambo yote unayohitaji yamo ndani yako. Kwa hiyo, basi, wewe anza tu kunywa kutoka katika ahadi ya Mungu, ukisema, "Ni kweli. Mungu alisema angeniponya. 'Kwa mapigo Yake mimi nimeponywa.'" Haya basi. Unaajua unalofanya? Unaanza kuusukuma uponyaji, hivyo tu. Unaona? Halafu basi, wengine wanawenza kuona ulicho nacho.

<sup>31</sup> Sasa kile ilicho, "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo; bayana ya mambo yasiyoonekana."

<sup>32</sup> Huenda nikauweka huo mti mdogo huko nje. Siyaoni matofaa, bali yamo mle ndani. Maskini huo mti mdogo unajua yamo mle ndani. Kwa hiyo yeche anaanza tu kunywa, kusukuma

na kusukuma, maana anajua, "Yamo ndani yangu. Nitayatoa hapa nje baada ya kitambo kidogo. Nipe muda mfupi. Nipe tu muda mfupi." Yeye anaendelea tu kunywa. "Naam, ninajua matofaa yamo ndani yangu. Nitayatoa, baada ya kitambo." Na muda si mrefu wajua, haya hapa yanakuja. Haya hapa matofaa yanakuja, kwa sababu aliamini ya kwamba yalikuwa ndani yake.

<sup>33</sup> Na kama unaamini ya kwamba uweza wa Roho Mtakatifu umo ndani yako, kukuponya, haya basi. Endelea tu kusukuma. Unaona? Una imani. Huwezi kuona matokeo yake mara moja. Huyaoni.

<sup>34</sup> Sasa, unaona, Yakobo alimhesabia haki Ibrahimu kwa kazi zake. Paulo alimhesabia Ibrahimu haki kwa imani yake. Tuseme nini basi, kati ya hao wawili? Ibrahimu alikuwa akinena juu ya yale...Ninamaanisha, Paulo alikuwa akinena juu ya yale Mungu aliyoyna katika Ibrahimu. Naye Yakobo alikuwa akinena juu ya yale watu walijoona katika Ibrahimu. Mnaona? Sasa, mnaona?

<sup>35</sup> Kwa hiyo, Mungu alijua kwamba, kabla ya mtoto huyo kuja, ya kwamba Ibrahimu alikuwa na imani. Naye Ibrahimu akalithibitisha kwa Mungu, kwa kutenda kama (yeye) kwamba mtoto atakuja wakati akiwa ni tasa. Yeye hakuwa na watoto. Tumbo la uzazi la mke wake lilikuwa limekuwa, naye alikuwa ni tasa. Lakini, hata hivyo, ye ye alijua, "Mle ndani mahali fulani kulikuwako na mtoto mchanga." Unaona, ye ye aliendelea kuinywa ile ahadi, ariegemea kwenye El-Shadai kuu la Mungu, lile *Ziwa*. Ariegemea pale, akinywa, akiju ya kwamba Mungu angempa; alijua kwamba ilikuwa ni ahadi, na Yeye ilibidi alifanye.

<sup>36</sup> Nasi ni watoto wa Ibrahimu. Kwa hiyo hebu na tuegemee kwenye ahadi Yake, na kushikilia pale, tukijua ya kwamba Mungu atafanya jambo hilo. Yeye alisema hivyo. Mnaliyamini sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

<sup>37</sup> Basi hebu wagonjwa na wapange mstari hapa kwenye moja ya pande hizi ama huo mwengine, wanaotaka kuombewa. Na kama tukimleta mzee hapa awapake mafuta, nitawaombea, na tutaamini ya kwamba Mungu atampa afya kila mmoja wao. "Kama unaweza kuamini."

<sup>38</sup> Teddy, uko wapi? Njoo huku upande wa mkono wa kuume. Hilo ni jema. Nami ninataka upige *Amini Tu*.

<sup>39</sup> Na wakati wakija, hebu na tuviinamishe tu vichwa vyetu, wasikilizaji wengine wote, na hebu tuwe katika maombi kwa ajili ya hawa watu wanaokuja.

<sup>40</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe, asubuhi ya leo, katika Jina la Yesu Kristo, maskini wanadamu hawa wagonjwa, wanaoteseka walio katika hali hii ya kutisha, ya maangamizi. Ninakuamini Wewe, Bwana. Ni-ninajua ya kwamba Maneno

Yako ni ya kweli. Ni ya kweli sana! Hayawazi kushindwa, kwa sababu ni Neno la Mungu la Milele na lisilo na mwisho. Yana nguvu zote, kama vile Mungu alivyo, kwa kuwa ni sehemu Yake. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwa kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa mionganoni mwetu.” Sasa, tunaamini hilo, Bwana, kwa mioyo yetu yote, kwa nafsi yetu yote, kwa yote yaliyo ndani yetu. Tunaliamini.

<sup>41</sup> Nami nimejaribu, katika njia rahisi, kama ya kitoto, kuliwasilisha kwa watu hawa, wapate kuelewa na kujuja ya kwamba Nguvu za Mungu zimo ndani yao. Laiti wangaliweza tu kuwa na imani yao na kuyaafuata maagizo ya Mungu.

<sup>42</sup> Hivyo ndivyo walivyookolewa. Walikuja na kutubu dhambi zao, nao wakabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kulingana na Biblia hii, Matendo 2. Ndipo basi Petro akasema, ya kwamba, “Mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Nacho hiki hapa kinakuja, vivyo hivyo hasa, kwa maana ni Neno la Mungu lililodhihirishwa.

<sup>43</sup> Vema, sasa, jambo lile lile, Baba, tunajua ni kweli, tunapowapaka wagonjwa mafuta, na kuwaombea. “Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa. Mungu atawainua.” Mungu, jalia kila mmoja aondoke kwenye madhabahu haya, karibu na mahali hapa asubuhi ya leo, wakiwa na furaha sana na kushangilia, katika kujuja ya kwamba Mungu amewaponya. “Nenda, ukaponywe.” Kwa kuwa tunawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo.

<sup>44</sup> Jalia kila mmoja aponywe, na apate ono, kile linachomaanisha. “Kama vile Ibrahimu, alivyoviita vitu hivyo, ambavyo havikuwapo, kama kwamba vilikuwapo.” Haidhuru matokeo yake ni nini, hilo halina uhusiano wowote na imani. Matokeo si kitu. Imani tayari imeshika. “Nayo imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, na ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Mungu, jalia lizame ndani katika mioyo yao, kwa kuwa wanakuhitaji Wewe.

<sup>45</sup> Ninaenda kama mtumishi Wako mnyenyeketu, kusimama hapa pamoja na watumishi wengine, na kumwomba Mungu aliweke moyoni mwetu kwa ajili ya watu hawa wagonjwa. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

<sup>46</sup> Mtu fulani alisema Ndugu Estle Beeler alikuwa humu jengoni. Nami ninaamini kuna mhudumu mwinge hapa, aliyeongoza katika maombi, asubuhi ya leo. Tunetaka kuwaliza wahudumu wote hapa, chochote kile walicho, kama ungeweza kupanda hapa juu na kusimama kuyazunguka madhabahu haya pamoja nasi, kwa muda mfupi tu, kidogo, tafadhalini, ndugu. Na hao wanaume... Ndugu Ben, asante. Njoo huku moja kwa moja na usimame hapa karibu,

kuyazunguka madhabahu hapa, tupate kuomba pamoja na hawa watu, kuwawekea mikono.

<sup>47</sup> Sasa, wakati wanapoupiga huo wimbo. Nao wahudumu wanachukua mahali pao hapa, kusudi sisi, kila mmoja, aweze kuweka mikono juu ya wagonjwa.

<sup>48</sup> Hebu tuone, akishuka kule mlimani. Namwona Mtu akija, hakuwa tofauti na mtu mwингine yejote. Yeye alikuwa ni Mtu wa kawaida tu, kidogo ana mwili mdogo, kidogo amedhoofika. Tunapomwona akiangalia, macho yake yameinamishwa kwenye ta—tamasha inayotukia huko chini bondeni. Ilikuwa ni mitume Wake. Walikuwa na mvulana kule chini, aliyekuwa na kifafa, na hapana shaka ila walikuwa wakisema, “Mponye, Bwana! Mponye!”

<sup>49</sup> Lakini, unaona, kusema tu, “Mponye, Bwana, mponeye,” halitasaidia. Hilo kamwe halitasaidia. Inapaswa kuwapo na kitu fulani nyuma ya hilo, “Mponye, Bwana, mponeye.” Mnaona? Na kama ninaweza kuwafanya mwamini hilo, na kuamini hilo kwa moyo wenu wote, mtaponywa, kama kweli nikiwafanya kuona hilo ono.

<sup>50</sup> Sasa angalieni, hao wanafunzi wakisimama pale, labda wakimtikisa, labda kumsukuma kwa nguvu zaidi. “Amini, ndugu! Amini! Haleluya! Amini! Mponye, Bwana! Mponye!” Lakini ibilisi alikaa pale pale, kwa kuwa asingeweza kupata imani ya kutosha hapo kumfanya aondoke.

<sup>51</sup> Lakini huyu hapa Mtu anashuka kutoka kilimani. Na mara huyo ibilisi alipotambua huyo alikuwa tofauti kidogo na wanaume hao wengine... Unaona?

<sup>52</sup> Sasa, hao ndio namna ya wanaume tunaotaka wawe hapo, kama Bwana wetu Yesu. Naam. Sio kuja tu kwa onyesho, bali kuja, mpende Mungu wetu, fahamu ya kwamba tumeagizwa kwenda kufanya jambo hili. Hili ni agizo letu.

<sup>53</sup> Halafu, wakati alipoenda kwa baba. Nafikiri hapa ndipo huu wimbo ulipoandikiwa, ulipotungwa kwa Neno. Yeye alisema, “Bwana, umrehemu mwanangu, maana amepagawa na ibilisi.” Kasema, “Yeye humtupa motoni, naye anazimia, na kadhalika.” Akasema, “Nilimleta kwa wanafunzi Wako, bali wasingeweza kumponya. Lakini ni—ni—nilifikiri...”

<sup>54</sup> Akasema, “Ninaweza, kama utaamini. Sasa, nina Uweza ndani Yangu,” Yeye akasema, “kufanya hilo, kama unaweza kuliamini.”

<sup>55</sup> Je! Mungu angeweza kuruhusu hao watu waliolemewa na kansa wanaoketi hapa asubuhi ya leo, ambao wamelazwa, wamelazwa kitandani kwa kansa, na lukemia, maradhi, mateso, hivi Mungu angewaponya na kukupita? Haiwezekani. La. Mnaona? Sasa, Yeye hashindwi. “Ninaweza, kama ukiamini.” Yeye alisema nini?

Kwa kuwa mambo yote yanawezekana, . . . tu  
 Sasa, Ndugu Tyler, njoo huku juu . . . ? . . .

Sasa amini tu, amini tu,

<sup>56</sup> Sasa, wakati ninapoomba, ninawatakeni muwawekee watu mikono. Chochote wanachohitaji, . . . ? . . . na mshuke moja kwa moja kwenye mstari.

<sup>57</sup> Ndugu Neville, wewe wapake mafuta, nao ndugu hawa . . . ? . . .

<sup>58</sup> Namtaka kila mtu, kwenye wasikilizaji, huku umekiinamisha kichwa chako sasa. Kila mtu katika kilindi cha maombi.

Amini . . .

<sup>59</sup> Bwana, turehemu, ninaomba, na ukawaponye watu hawa, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

Katika Jina la Yesu wa Nazareti . . . ? . . .

<sup>60</sup> [Ndugu Branham na wahudumu wanaomba na kuwawekea mikono wagonjwa, wakati Ndugu Neville akiwapaka mafuta. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>61</sup> Wengi sana, mstarini, ninawaangalia, kuona wanavyochukulia jinsi walivyokuwa, kuona jinsi wanavyojibu tendo likifanyika. Mnaona? Kuna kitu kama tendo, wao walismama na kuja mbele. Jambo lingine, ni jinsi wanavyolichukulia tendo hilo ambalo wametenda. Baada ya kufikia mahali pa kuaminia, kwamba, wakati wanapoombewa, wangeponywa, basi angalia watakalotenda baada ya tendo hilo lao.

<sup>62</sup> Sasa, mchungaji wetu ana ujumbe mzuri kwa ajili yetu, nina hakika, asubuhi ya leo.

<sup>63</sup> Jambo moja ningetaka kulitolea maoni kwa muda mfupi tu, palikuwapo na msichana Mkataliki aliyesimama pale karibu na madhabahu. Siku chache zilizopita alikuwa nyumbani kwangu, ye ye pamoja na mume wake. Nami nimemfahamu mumewe kwa kitambo kidogo. Na—na kulikuwako na kitu kilichotukia wakati tulipokuwa tumeketi kwenye mazungumzo ya faragha.

<sup>64</sup> Hapo ndipo tulipokuwa na ono lile. Hapo ndipo sisi . . . Nilizoea kuyafanyia hapa kanisani, lakini yakachukua asubuhi yote, na kadhalika. Na kwa hiyo ilikuwa ni huko ndani.

<sup>65</sup> Kamwe sikusema kitu, kwa kuwa ye ye akiwa ni msichana, jambo lingine, daima alilelewa katika kanisa Katoliki, na kadhalika. Lakini alienda kuzungumza kwa niaba ya mama yake. Na kwenye wakati huo, niliona ono la mama yake. Nikamwambia shida ya mama yake ilikuwa ni nini, na kutoa wasifu wake, na umbo la mama yake. Hakika, alikuwa mwamuzi wa hayo, kama yalikuwa ni kweli ama si kweli. Kamwe sikuwa nimemwona mama yake, maishani mwangu. Yeye anajua hilo.

<sup>66</sup> Naye msichana huyo, asubuhi ya leo, alikuja hapa madhabahuni na kusimama, kuungama, na kumkubali Kristo kama Mwokozi wake. Alifanya hivyo madhabahuni, asubuhi ya leo.

<sup>67</sup> Ndugu Neville, bila kujua, alimpaka mafuta. Jinsi—jinsi Mungu anavyofanya kazi! Alimpaka mafuta, kwa ajili ya ugonjwa. Lakini angalia matendo ya Roho Mtakatifu. Sasa, kwa kuwa alipakwa mafuta, kweli si mgonjwa, bali amepakwa mafuta. Unaona jinsi linavyofanya kila kitende kazi sawasawa? Yeye alisimama kama Mkristo sasa, baada ya yeye kuwa kile tunachoamini ni Mkristo. Sasa, akasema, "Waweza kumwombea mama yangu? Yeye ni mgonjwa." Huyo ni yule yule. Kwa hiyo mafuta ya kupakwa yalitumiwa mapema. Nikawaza, jinsi livilyo muafaka, kwamba, mnaona, mtu akiisha tu kuokolewa. Kristo alituwakilisha sisi sote. Yeye huwakilisha wote. Na mara msichana huyu alipokuwa Mkristo, basi anataka kumwakilisha mtu fulani, pia, ikionyesha ya kwamba Roho wa Kristo huingia ndani yetu wakati tukiwa kweli tumeokolewa. Sasa, hilo ni zuri kweli. Ha—hakika ninalithamini hilo, hiyo Roho nzuri ya Kikristo ya kuamini. Sasa, kumbukeni tu.

<sup>68</sup> Sasa, kwa msichana huyu mdogo, yeye yuko hapa mahali fulani, na kwa mama mwingine Mkatoliki aliyejuka hapa. Nami ningetaka kusema maneno haya, kabla tu sijamwachia mchungaji wetu ibada, mnaona, ni hili. [Ndugu Neville alisema, "Amina."—Mh.]

<sup>69</sup> Sasa, kanisa Katoliki lilikuwa wakati mmoja kama kanisa hili. Kama utarudi nyuma na kuisoma Biblia, ambayo tunaiamini, nanyi mnajua ya kwamba Kanisa Katoliki lilikuwa ndilo Kanisa la kwanza. Hiyo ni kweli. Lakini liliyaacha Mafundisho Yake. *Hili* lilikuwa ndilo fundisho la kanisa Katoliki. Lakini, mnaona, wana vitabu vingine mia sita na kitu ambavyo mapapa na kadhalika walikuwa wameandika, ambavyo ni vitakatifu kwao kama tu hii Biblia.

<sup>70</sup> Kwa hiyo, unaona, kile hili lilicho, hujabadilika. Kile umefanya, ndio kwanza uongoke. Unaona? Sasa kama ukichukua... Hakika, nadhani labda baadhi yenu, hao wawili, asubuhi ya leo, walikuwa ni wanawake. Huenda kukawa na wanaume Wakatoliki walioketi hapa.

<sup>71</sup> Ikiwa utarejea kwenye historia ya kanisa, kama huenda ukamwuliza kasisi wako, "Matendo ya hawa mitume katika Biblia hapa, ilikuwa kwamba njia ambayo... Hao walikuwa Wakatoliki wa mwanzoni?" Yeye atasema, "Ndiyo." Na hiyo ni kweli. Walikuwa ndio. Sasa, wao, angalia ni dini ya aina gani waliyokuwa nayo. Walikutana mahali padogo, rahisi. Kamwe hawakusema, "Salamu Maria" ama "Baba yetu" Hayo ni mapokeo ya kanisa. Wao walisema nini? Walimsifu Mungu. Walipiga makelele. Walilia.

<sup>72</sup> Angalieni hapa katika Matendo 2, wakati Mtume mtakatifu Petro, na Yakobo, na Yohana, na wote walikuwa pamoja. Biblia ilisema walinenia kwa lugha. Nao wakapiga makelele, na hata walitenda kama waliojazwa na Roho sa—sana hata wakafanya kama walevi, na hata mpaka ulimwengu wa nje ukauliza, “Hawa wote si wamelewa?”

<sup>73</sup> Ndipo Petro, yule mtume, yule mtawa Mtakatifu Petro, wakati aliposimama, naye akasema, “Wanaume na ndugu zetu, hawa watu hawajalewa, bali wamejazwa na Roho,” kama ninii—kama Biblia ilivyosema walikuwa. Sasa, hilo lilikuwa ni kanisa Katoliki la mwanzoni, kulingana na mafundisho yao.

<sup>74</sup> Sasa, unaona, baada ya karibu miaka mia mbili, waungwana walianza kuingia kanisani. Basi walifanya nini? Waliunda dhehebu lao la kwanza katika Baraza la Nikea, A.D 606. Walifanya ninii yao... Wakati Baraza la Nikea liliopokutana huko Nikea, Rumi, walianza kuwaingiza waungwana wote, nao *wakaunda* tu kanisa, na *kufanya* kanisa.

<sup>75</sup> Baada ya hapo, livilunjika mara nne ama tano. Waliondoka—waliondoka kutoka hapo, wakaenda kwa askofu; kutoka kwa askofu, hadi kwa papa. Na kutoka hapo, likaja la Othodoksi ya Kiyunani na mengine mbalimbali, mpaka yakavunjika tu, kufikia ambapo mnalionia leo hii. Liko tu katika kila namna ya kutengana.

<sup>76</sup> Lakini kile tunachojaribu kufanya, rafiki yangu Mkatoliki, unaona, sisi ni katoliki, pia. Sisi ni wale wa mwanzoni, katoliki ya mwanzoni. Na kanisa wanaloituita sasa, zaidi sana, tunatajwa kama pentekoste, kwa sababu tunaamini katika baraka za kipentekoste.

<sup>77</sup> Hapo ndipo kanisa Katoliki lilipojiundi dhehebu. Na katika madhehebu yetu ya Kipentekoste, leo, kama—kama ulimwengu huu ungesimama miaka mia tano zaidi, dhehebu hili la Kipentekoste lingekuwa baridi kuliko kanisa Katoliki la Kirumi liliyuo leo. Linaenda tu mbali zaidi, njia ile ile. Na wanapounda dhehebu, wanafanya chama kutokana nalo. Ndipo wanakuwa tu ni chama, na wanachama, na watu wasioongoka.

<sup>78</sup> Kwa wapendwa ndugu na dada zangu, wa thamani, kwenu nyote. Kama mtumishi wa Mungu, sijawahi kusema jambo hili hapo kabla, ulimwenguni, katika kanisa hili, kamwe sijasema. Lakini kama nabii wa Bwana, ninawaambia, “Hii ndiyo Nuru. Tembeeni ndani Yake.” [Kusanyiko linashangilia na kusema, “Amina.”—Mh.]



*IMANI* SWA61-0813  
(Faith)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 13 Agosti, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila jithada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)